**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**
**Tovuti:** www.hlpc.go.tz
Simu: **0734005777/ 0750059900**

# TAARIFA KWA UMMA

## USHIRIKI WA BARAZA KWENYE KONGAMANO LA 38 LA WATAALAM WA MAABARA MKOANI MWANZA

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inapenda kuwataarifu Wataalam wote wa Maabara nchini kuwa Baraza la litashiriki katika kongamano la Kisayansi la Wataalam wa Maabara litakofanyika Jijini Mwanza-**kwatunza Beach** kuanzia tarehe 24.09.2025 hadi 26.09.2025. Kongamano hili linaratibiwa na kusimamiwa na Chama cha Wanasayansi wa Maabara za Afya (MeLSAT).

Shughuli zote za Baraza zitahamia kwa muda Jijini Mwanza-**kwatunza Beach**
Kwa siku zote. Hivyo, Msajili anawaalika Wataalam wote kutembelea Banda la Baraza la Wataalam wa Maabara kuanzia tarehe ya kuanza kongamano hadi mwisho ili kupata huduma, kujifunza na kujua shughuli mbalimbali zinazotolewa na Baraza.

Wataalam wa Maabara mnaalikwa kushiriki kwa wingi katika kongamano hili muhimu ambapo Wataalam wa Maabara watakaoshiriki watapata alama kumi (10) za mafunzo endelevu (10 CPD Points)

Ofisi ya Msajili inawatakia ushiriki mwema

Imetolewa na
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
22.09.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
22 SEP 2025
P.O.Box 743
DODOMA